BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

RIPOTI YA KAMATI YA KUDUMU YA KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO YA BARAZA LA WAWAKILISHI

FEBRUARI, 2018

BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

RIPOTI YA KAMATI YA KUDUMU YA KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO YA BARAZA LA WAWAKILISHI

RIPOTI YA KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

SEHEMU YA KWANZA

1. UTANGULIZI

Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar ni Kamati ya Utawala, Nidhamu na Uchumi ambayo imeundwa chini ya kanuni ya *106* ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, (Toleo la mwaka *2016*). Kamati hii ni mpya kiutendaji kwani imeanza kufanya kazi rasmi katika mwaka 2017. Kwa mujibu wa *Jaduweli la Kwanza* la Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Kamati hii inatekeleza majukumu yafuatayo:

(a) Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia;
(b) Kuchambua Kanuni na Sheria ndogo ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa ya masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyengine za nchi;
(c) Kujadili na kutoa mapendekezo kwa Taasisi husika juu ya namna bora ya kutengeneza Kanuni na Sheria ndogo;
(d) Kulishauri Baraza kupitisha azimio la kubatilisha Kanuni au Sheria ndogo ambazo zinakiuka masharti ya Katiba, Sheria Mama au Sheria neynginezo za nchi;
(e) Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

1.1 MUUNDO WA KAMATI

Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar ina jumla ya Wajumbe *saba (7)* wafuatao:

Nam.	Jina	Wadhifa
1.	Mhe. Rashid Makame Shamsi	Mwenyekiti
2.	Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Mohammed Said Mohammed	Mjumbe
4.	Mhe. Shaib Said Ali	Mjumbe

5.	Mhe. Zulfa Mmaka Omar	Mjumbe
6.	Mhe. Ame Haji Ali	Mjumbe
7.	Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Mjumbe

Aidha, Kamati inatekeleza majukumu yake chini ya makatibu *wawili (2)* wafuatao:

Nam.	**Jina**	**Wadhifa**
1.	Ndg. Khamis Hamadi Haji	Katibu
2.	Ndg. Haji Jecha Salim	Katibu

SEHEMU YA PILI

2. SHUGHULI ZILIZOFANYWA NA KAMATI

Kuanzia tarehe *28 Agosti* hadi *01 Septemba, 2017*, Kamati iliendelea na shughuli zake mbalimbali ikiwemo kupatiwa mafunzo juu ya mambo mbalimbali ya msingi ambayo yataisaidia Kamati hii katika utekelezaji wa majukumu yake. Ripoti imeeleza kwa ufupi shughuli zilizofanywa na Kamati katika kipindi hiki kama ifuatavyo:

2.1 MAFUNZO KWA WAJUMBE WA KAMATI

Katika kuwajengea uwezo wajumbe, Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo imepata mafunzo mbali mbali katika vipindi viwili tofauti. Lengo la mafunzo hayo yalikuwa ni kuwapa uwelewa wajumbe wa Kamati juu ya mambo mbali mbali yanayohusu Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo ili kuwawezesha katika utendaji kazi zao.

2.2 **Yafuatayo ni miongoni mwa mambo muhimu ambayo wajumbe walijifunza katika mafunzo hayo:-**

i. Maana na aina za Sheria ndogo ndogo.
ii. Kazi na majukumu ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo ya Baraza.
iii. Mambo ya Kuzingatia katika utungaji wa Kanuni na Sheria ndogo ndogo.
iv. Uzoefu wa baadhi ya Mabunge ya Jumuiya ya Madola katika kusimamia utengenezaji (utungaji) wa sheria ndogo ndogo.
v. Chimbuko na uzoefu wa Kamati ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika utendaji wa kazi zao.
vi. Mazoezi ya Vitendo ya kupitia Sheria na kufanya uchambuzi wa Kanuni.

2.3 UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA SABA WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANIZIBAR

Katika Mkutano wa Saba wa Baraza la Tisa la Wawakilishi uliofanyika kuanzia tarehe *27 Septemba, 2017* na kumalizika tarehe *12 Oktoba, 2017*, jumla ya Kanuni *mbili (2)* zifuatazo ziliwasilishwa:

(a) Kanuni za Huduma Zinazotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
(b) Kanuni za Mirathi ya Kiislamu.

Kamati ilipanga kuzifanyia kazi Kanuni hizo ili kuendelea kujijengea uwezo kiutendaji na kiufanisi katika kuhakikisha kuwa itaweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo katika vipindi vyengine ambapo uwasilishaji wa Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo katika Baraza utakapoimarika. Kanuni hizo hazikupitiwa kwa madhumuni ya Kamati kuzitolea azimio ndani ya Baraza endapo zingebainika na makosa, bali katika utaratibu wa kujenga uwezo zaidi. Mambo kadhaa yalionekana na Kamati wakati wa kuzipitia ambayo Kamati imekaa na Wizara husika na kujadiliana nao na hatimaye Wizara imekubaliana na Kamati kuyafanyika kazi.

2.3.1 ZIARA ZA KAMATI KATIKA TAASISI ZINAZOHUSIANA NA UTUNGAJI WA KANUNI

Kamati, kabla ya kuanza kuzichambua Kanuni hizo, ilifanya ziara ya kimafunzo katika taasisi za Serikali ambazo kwa njia moja au nyengine zinahusiana au zinahusika na taratibu za utungaji wa Kanuni kwa lengo kuu la kujifunza pamoja na kufahamu mambo mbalimbali yanayohusiana na utungaji wa Sheria na Kanuni. Taasisi hizo ni hizi zifuatazo:

(a) **Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

Kamati ilitembelea Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa lengo la kukutana na uongozi wa Afisi pamoja na watendaji wa Kitengo cha Uandishi wa Sheria na Kanuni ambacho kimeundwa na watu *saba (7)*. Ziara hiyo ya Kamati

ilikuwa na lengo la kufahamu hatua mbalimbali wazazopitia katika kutunga Sheria na Kanuni hizo.

Kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka *1984*, Afisi ya Mwanasheria Mkuu ndiyo yenye jukumu la kutunga, kuandaa na kuratibu masuala yote yanayohusiana Sheria na Kanuni nchini. Kanuni hutungwa kwa ajili ya utekelezaji bora wa sheria mama na hutungwa kwa mujibu wa mipaka yake bila ya kukiuka Katiba, sheria mama, sheria nyengine pamoja na Kanuni nyengine.
Kwa kuzingatia majukumu ya Kamati, hii ni sehemu nzuri ambayo itafanikisha utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

Mara tu baada ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kupitishwa sheria, Afisi ya Mwanasheria Mkuu huikumbusha Wizara husika juu ya matumizi ya sheria hiyo pamoja na wajibu wa kutunga Kanuni. Hii inatokana na kuwa utekelezaji wa baadhi ya sheria hushindwa kutekelezeka ipasavyo kutokana na kukosekana kwa Kanuni.

(b) **Wakala wa Serikali wa Uchapishaji Zanzibar**

Wakala wa Serikali wa Uchapishaji Zanzibar ni Taasisi ya Serikali yenye jukumu la kuchapisha miswada ya sheria na sheria, machapisho yote ya wizara na taasisi za Serikali, machapisho yake pamoja na taasisi binafsi na kufungua Bohari ya Kuu ya vifaa vya ofisini.

Nyaraka nyingi zinazochapishwa na Wakala kutoka Serikalini huwasilishwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambapo hupelekwa kwa mtiririko wa namba maalum.

CHANGAMOTO

Wakala inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(a) baadhi ya wakati, wizara/taasisi hushindwa kulipa au kuchelewa kulipa.
(b) kufanyishwa kazi kwa uharaka ambapo hupelekea kutokea kwa kasoro katika kazi hizo.

Kwa mantiki ya majukumu ya Kamati, Wakala ni mdau mkubwa kwa vile ndio yenye jukumu la kuchapisha Sheria na Kanuni zinazotungwa na wizara/taasisi mbalimbali za Serikali.

(c) **Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar**

Kamati ilitembelea Tume ya Kurekebisha Sheria Zaznibar na kuelezwa namna inavyotekeleza majukumu yake ikiwemo kufanya utafiti kabla na wakati wa kuzifanyia mapitio sheria mbalimbali nchini.

Mambo yafuatayo yaliwekewa msisitizo:

(i) Kanuni ni vyema zikaambatana na sheria husika kama ilivyokuwa hapo zamani ili kuepusha changamoto zinazojitokeza hapo baadae ikiwemo kutokutekelezeka kwa baadhi ya vifungu vya sheria hizo.
(ii) Msisitizo ulitolewa kwamba ni vyema kabla ya kutunga Kanuni au Sheria kufanya utafiti wa kina utakaopelekea kufahamu mahitaji halisi ya jamii husika. Kwani kutunga sheria/kanuni zisizozingatia mawazo ya jamii na mazingira yao husababisha wananchi kutozifuata ipasavyo mfano kukwepa kulipa ada/tozo.
(iii) Serikali itunge sheria kwa utaratibu mzuri na kuepuka kutunga sheria zisizoweza kutekelezeka kwani baadhi ya mambo yanahitaji kutolewa elimu kwa jamii kabla sheria kutungwa.
(iv) Kuna umuhimu kwa watunga sera, sheria na kanuni washirikishwe katika hatua zote zinazostahiki ili kuepuka kuwepo kwa mawazo tofauti.

(v) Wizara/taasisi za Serikali zishirikiane wakati wa kutunga sera, sheria na kanuni kwa ajili ya kuepuka migongano isiyo ya lazima.

2.3.2 MIKUTANO NA WADAU WA KANUNI

Vilevile, Kamati ilikutana na wahusika mbalimbali ambao wamegawika katika sehemu kuu *mbili* zifuatazo:

(a) **Taasisi za Serikali**

Kamati ilitembelea katika taasisi za Serikali zifuatazo: **Baraza la Manispaa Mjini; Baraza la Manispaa Magharibi 'A'** na **Baraza la Manispaa Magharibi 'B'** ambazo miongoni mwa majukumu yao ni kukusanya mapato ya Serikali yanayostahiki kukusanywa kwa mujibu wa Kanuni za Huduma Zinazotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizotungwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, nambari *7* ya mwaka *2014*. Kamati ilitaka kufahamu mambo yafuatayo:

(i) Muundo wa Mabaraza hayo;
(ii) Utekelezaji wa Majukumu ya Mabaraza hayo;
(iii) Taratibu wanazotumia kutunga Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo;
(iv) Ushirikishwaji wa Mabaraza hayo wakati zilipotungwa Kanuni za Huduma zinazotolewa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Mitaa, nam. *7* ya *2014*;
(v) Mahusianao yaliopo baina ya Baraza la Manispaa na Wakala wa Serikali wa Uchapishaji Zanzibar;
(vi) Mazingatio yanayochukuliwa na Mabaraza ya Manispaa wakati wa utungaji Kanuni na Sheria Ndogo juu ya viwango vya ada;
(vii) Changamoto zinazokabili Mabaraza ya Manispaa katika utekelezaji wa Kanuni na Sheria Ndogo.

Kamati, wakati wa majadiliano na taasisi hizo ilibaini kwamba, zimefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika utekelezaji wa majukumu yao lakini pia, zinakabiliwa na changamoto zinazofanana kama ifuatavyo:

(i) Kuchelewa kutungwa kwa Kanuni za Huduma zinazotolewa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kumepelekea Mamlaka hizo kushindwa kutunga sheria ndogo.
(ii) Uhaba wa wataalamu katika kutekeleza majukumu yao kama yalivyoanishwa kwenye Sheria na Kanuni.

(b) **Taasisi zisizo za Kiserikali**

Taasisi zisizo za Kiserikali ziliwakilishwa na wawakilishi wao ambapo Kamati ilitaka kupokea maoni yao juu ya Kanuni zilizotungwa na ambazo zinatumiwa kwa kiasi kikubwa na taasisi zao. Wawakilishi hao kwa upande wao waliweza kuwasilisha maoni na mapendekezo yafuatayo:

(i) Kufanyiwa marekebisho ya kiuandishi katika baadhi ya vifungu vya kanuni.
(ii) Viwango vya adhabu kwa makosa mbalimbali vipunguzwe hasa kwa kuzingatia kwamba watumiaji/wahusika wengi wa Kanuni hizi ni masikini mfano wajasiriamali wadogo, mama na baba lishe, watembeza bidhaa, wavuvi n.k
(iii) Baadhi ya viwango vya ada/tozo ni vikubwa, mazingatio yanahitaji kufanywa kwa kutazama hali halisi ya maisha.
(iv) Serikali ipunguze wingi wa ada/tozo ambazo hutozwa na taasisi mbalimbali za Serikali kwa mtu mmoja na kwa kitu kimoja. Hali hii hupelekea utozaji wa ada/tozo kwa mara *mbili*. Hili hujitokeza sana katika ada/tozo zinazohusiana na biashara, maliasili, kilimo, mawasiliano na taasisi nyengine zikiwemo Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB). Hivyo, iwapo kuna umuhimu wa kubakia kwa

ada/tozo hizo ni vyema zikaunganishwa pamoja ili kuleta unafuu na kuondoa utozaji wa mara *mbili* pamoja na kuondoa urasimu.

(v) Serikali ihakikishe kuwa inatoa elimu kwa jamii (mijini na vijijini) ili iwe rahisi kutekeleza mipango ya Serikali husan katika utunzi wa Kanuni.

(vi) Jamii ishirikishwe ipasavyo wakati wa kuandaa mipango ya Serikali hususani ile inayoigusa jamii *moja* kwa *moja*.

(vii) Serikali ihakikishe kuwa inasimamia vizuri ukusanyaji wa mapato hayo na iwapo haijajipanga, ni vyema ikatafuta wakala wa ukusanyaji kufanya kazi ya ukusanyaji kwa utaratibu maalum wa kuingia mkataba.

(viii) Kanuni ziandaliwe kwa lugha nyepesi na rafiki ambayo haitakuwa vigumu kufahamika katika jamii zinakotumika.

(ix) Wasimamizi wa Kanuni hizi kutoka Serikali za Mitaa wapewe kipaumbele kuzielewa Kanuni hizo ili waweze kusimamia vyema utekelezaji wake.

2.3.3 KANUNI ZA HUDUMA ZINAZOTOLEWA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA, 2017

Kamati katika kuendelea na utekelezaji wa majukumu yake, ilipitia na kuzichambua *Kanuni za Huduma Zinazotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa* za mwaka *2017* ambazo zimetungwa chini ya kifungu cha *94* cha *Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mtaa, nambari 7 ya 2014*. Sheria hii imempa uwezo *Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za* SMZ kutunga Kanuni hizi. Baada ya kufanya mapitio kamati iligundua kwamba, Kanuni hizo zina kasoro kadha za Kiuandishi, kimantiki na kiada.

2.3.3.1 Baadhi ya kasoro za jumla zilizogunduliwa ni kama ifuatavyo:

(a) Utaratibu uliotumika kutunga Kanuni hizo

Ushirikishwaji wa wahusika/wadau wakiwemo wananchi wanaotarajiwa kwa kiasi kikubwa kutumia Kanuni hizi uliokuwepo ila si kwa kiwango kikubwa. Hivyo, Kamati imeishauri Wizara kwa mara nyengine itakapokuwa inatayarisha Kanuni au kitu chochote ambacho kinaihusu jamii, ni vyema ikaishirikisha jamii husika ili iwe rahisi katika utekelezaji wake.

(b) Vifungu vinavyohitaji kutungiwa Kanuni katika *Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, nam. 7 ya 2014*

Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, nam. 7 ya 2014 ina vifungu vingi ambavyo vinahitaji kutungiwa Kanuni mbali ya kifungu cha jumla cha 94. Hivyo, Kamati imeitaka Wizara kuhakikisha kwamba inatunga Kanuni kwa ajili ya vifungu hivyo iwapo kuna ulazima wa kufanya hivyo.

(c) Makosa ya kiuandishi na kiuchapaji

Kamati imebaini uwepo wa makosa mengi ya kiuandishi na kiuchapaji katika vifungu kanuni kadhaa ambapo Wizara imeahidi kwenda kuyafanyia kazi.

(d) Matumizi ya lugha isiyokuwa rasmi na ya mazungumzo.

Kamati imebaini matumizi ya lugha isio rasmi katika baadhi ya kanuni. Hata hivyo, Wizara imekubali kwenda kuyafanyia kazi ipasavyo.

(e) Ada/tozo ambazo bado zinatumika katika sheria za asili

Kamati imebaini uwepo wa ada/tozo ambazo bado zinaendelea kutumika katika Sheria zake za awali, kwa mfano: Sehemu ya Tano ya Kanuni imejumuisha "*Udhibiti wa Mazao ya Misitu*" ambayo bado yanatozwa katika sheria zake za asili hali inayopelekea kuwepo na malipo ya mara *mbili* kwa kitu kimoja na kusababishia mzigo kwa jamii.

(f) Mlingano sawia (consistence) wa maneno;
Kamati imebaini kuwa kuna baadhi ya maneno na vifungu vya maneno vilivyotumika mara kwa mara katika Kanuni hii havina mlingano sawia (consistence). Wizara imekubali kufanya marekebisho ili kuleta uwiano.

2.3.3.2 Mambo mengine makhsusi yafuatayo yaligunduliwa na Kamati katika *Kanuni za Huduma Zinazotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, 2017.*

Nam.	**Mapungufu**	**Maelezo ya Ufafanuzi**	**Kanuni inayohusika**
1.	Uwajibikaji	Kanuni zilizo chini ya Sehemu ya Pili inayohusiana na "Uhifadhi wa Mazingira na Ukusanyaji wa Taka" zimeweka wajibu wa mtu anayeishi katika eneo la Mamlaka kuweka safi mazingira na mambo mengine yanayohusiana. Hata hivyo, Kamati imeona kwamba, Mamlaka za Serikali za Mitaa nazo zina wajibu mkubwa wa kuweka safi mazingira kwani imekuwa ni jambo la kawaida kwa Mamlaka hizo kuweka taka katika masoko au mitaani kwa muda mrefu bila ya kuzichukuwa na kuzipeleka katika sehemu husika. Vilevile, suala la utunzaji wa mazingira kwa upande wa Mamlaka huonekana kuwa dogo pale wanapotaka kufanya shughuli maalum kama vile kuziba mashimo barabarani, huweka vifusi pembezoni mwa barabara na	Kuanzia kanuni ya *3*.

Nam.	Mapungufu	Maelezo ya Ufafanuzi	Kanuni inayohusika
		wanapomaliza shughuli zao hushindwa kuviondoa na kusababisha uchafuzi wa mazingira. Hivyo, Kamati imeishauri Wizara kutoa taaluma kwa Mamlaka/taasisi nyengine pamoja na wananchi juu ya umuhimu wa kuweka safi mazingira.	
		Kamati pia, imeonesha wasiwasi wake juu ya marufuku kwa vyombo na wanyama kupita kwenye njia za watu wanaokwenda kwa miguu ya kwamba katika nchi yetu hakuna njia zilizowekwa maalum kwa ajili ya kupita vyombo na wanyama, licha ya kuwa lengo la kanuni ya 28 ni kutenganisha mwingiliano kati ya binaadamu na wanyama.	Kanuni ya *28*.
2.	Migongano na Sheria au Taasisi nyengine	Kamati imegundua kwamba, baadhi ya kanuni zina migongano na sheria nyengine kama ifuatavyo:	

Nam.	Mapungufu	Maelezo ya Ufafanuzi	Kanuni inayohusika
		Sheria inayohusiana na Mazingira.	*(i)* Kanuni ya 9 inayohusiana na utupaji taka na maji machafu katika mitaro. *(ii)* Kanuni ya *24* na *26* zinazohusiana na uchimbaji mchanga.
		Sheria zinazohusiana na Ardhi.	Kanuni ya *53* inayohusiana na na ada ya uhaulishaji ardhi.
		Sheria inayohusiana na Leseni.	Kanuni zilizo katika Sehemu ya Tatu juu ya *"Utaratibu wa Utoaji wa Leseni za Biashara"*.
		Sheria zinazohusiana na Mawasiliano na Ardhi.	Kanuni za 62 na 63 zinazohusiana na ukodishaji wa ardhi kwa ajili ya ujenzi wa mnara pamoja na ada ya ujenzi wa mnara na uendeshaji.
		Sheria zinazohusiana na Kilimo na Usafirishaji.	Kanuni za *65*, *66* na *67* zinazohusiana na ada ya diko, usajili wa vyombo vya usafiri na uwekaji wa

Nam.	Mapungufu	Maelezo ya Ufafanuzi	Kanuni inayohusika
			kumbukumbu za usafiri wa majini vilivyo katika eneo la Mamlaka.
		Sheria zinazohusiana na Mifugo.	Kanuni zilizo katika Sehemu ya Saba inayohusiana na *"Udhibiti na Uzururaji wa Wanyama"*.
		Sheria ya Mtoto, nam. 6 ya 2011.	Kanuni ya 7 ambayo inayoelezea juu ya kumfanyisha kazi mtoto aliye chini ya miaka *18*.
		Sheria inayohusiana na Usafiri.	Kanuni zilizo chini ya Sehemu ya Nne inayohusiana na *"Huduma za Usafiri"*.
		Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake.	Kanuni ya *39(2)* ambayo imenakili Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake ila kanuni hiyo imeweka adhabu ambayo haimo katika Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma.

Nam.	Mapungufu	Maelezo ya Ufafanuzi	Kanuni inayohusika
	(a) adhabu kubwa na zisizofanana;	Makosa yanatofautiana.	Kanuni ya *30, 34(3), 44(2), 56, 61.*
	(b) adhabu ya kifungu katika maeneo yasiyo na ulazima.	Ada ya mazao ya misitu.	Kanuni ya *57(3), 59(2).*
	(a) Ada ya Ujenzi.	Fomu inayotakiwa kujazwa haimo katika Jaduweli.	Kanuni ya *54.*
	(b) Utaratibu wa mnyama aliyekamatwa.	Utolewe ufafanuzi juu ya kanuni hii kwani inaonekana kumkandamiza mwananchi mnyonge.	Kanuni ya *73.*
	(c) Maegesho ya Vyombo vya Moto.	Sehemu hii inahitaji ufafanuzi wa kutosha ili kuweka bayana mambo yafuatayo: ➢ Kuwe na tafsiri ya neno "maegesho" pamoja na vigezo vinavyotumika kujua iwapo chombo kimeegeshwa au vyenginevyo kwa lugha ya kiingereza 'stop' na 'parking'.	Sehemu ya Nane *"Maegesho ya Vyombo vya Moto".*

Nam.	Mapungufu	Maelezo ya Ufafanuzi	Kanuni inayohusika
		➢ Kukosekana kwa maeneo ya kuegesha magari; ➢ Vituo vya daladala; ➢ Utaratibu wa kupima muda katika maegesho; ➢ Wajibu wa Mamlaka pale kunapotokea uharibifu wa chombo au kuibiwa vifaa katika chombo ambacho kimelipiwa kihalali katika maegesho.	
	(d) Adhabu ya jumla.	Katika sehemu hii ya Nane inaonekana kuwepo kwa adhabu mbili (2) za jumla.	Kanuni ya *82* na *86*.
	(e) Utaratibu wa ukaguzi wa sehemu za biashara	Muda uainishwe ambao hautamvunjia mfanyabiashara haki zake za kibinaadamu.	Kanuni ya *38*.
3.	Mpangilio usioeleweka wenye utata a. vifungu cha Kanuni b. Jadweli	Sehemu ya Nne imejumuisha mambo mchanganyiko kinyume na kichwa cha habari. Jadweli ya malipo ya ada za huduma iliyo chini ya kifungu cha 87 cah Kanuni haipo katika mfumo mzuri kwa	*(a)* Kuanzia kanuni ya *49* hadi *52* zinazungumzia huduma za usafiri; *(b)* Kuanzia kanuni ya 53 hadi *55* zinazungumzia mambo ya ujenzi na ardhi.

Nam.	Mapungufu	Maelezo ya Ufafanuzi	Kanuni inayohusika
		walengwa. Baadhi ya maneno hayajakamilika. Baadhi ya ada zilizowekwa kutokuwa na uwiano mzuri na huduma inayotolewa.	
			Jaduweli.
4.	Makosa ya kiuandishi na kiuchapaji	Baadhi ya vifungu vingi vina makosa ya kiuandishi na kiuchapaji kiasi cha kubadili maana au ufasaha wa lugha ya Kiswahili.	Kanuni ya 2,4,5,8,9 (2),11,12 (2),20, 21, 26, 29, 30, 61 (2), 80, 85
5.	Kukosekana kwa mlingano sawia (consistence) kwa baadhi ya maneno au istilahi.	Baadhi ya maneno au vifungu vya maneno vimekosa mlingano an mengine yamekosa uasili wa matumizi	Mfano:- rikwama/mkokoteni, Vifungu vianvyotaja ada/faini, maji taka/maji machafu n.k

MAONI YA KAMATI JUU YA KANUNI ZA HUDUMA ZINAZOTOLEWA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

(a) Kabla ya kutunga Kanuni ni vyema taasisi zifanye utafiti wa kina juu ya kodi au ada inazotaka kuweka ikiwa ni pamoja na kuangalia uhalisia wa jamii husika.

(b) Kuwafikiria sana wananchi pamoja na hali ya maisha ambao ni walengwa wa Kanuni kwa kuangalia idadi ya ada/tozo ambazo wananchi wanalipa kwa kitu au huduma katika taasisi nyengine.

(c) Kuweka mazingatio ya kuihamasisha jamii kwa kuweka viwango vya ada/tozo ambazo wananchi wataweza kulipa badala ya kuweka kupata viwango vikubwa vya mapato ambavyo huwafanya wananchi kutafuta njia za kukwepa kulipa.

(d) Mamlaka ziaze kwanza kuimarisha na kutoa huduma stahiki kwa wananchi kabla ya kuwatoza ada/tozo wananchi kwa huduma zisizokuwepo.

(e) Mamlaka husika zianze kwanza kutokufanya yale ambayo wamewakataza wananchi kufanya kama vile kuweka ovyo kifusi au mawe pale wanapotaka kufanya jambo hususani pembezoni mwa barabara ambapo kikawaida huwa hawana utaratibu wa kuondoa. Vilevile, kuzoa au kuchukua taka katika maeneo yanayowajibikia kwa wakati.

(f) Mamlaka iwe na utaratibu maalum wa kuwashirikisha wadau husika wakati inapoandaa Kanuni.

2.3.4 KANUNI ZA MIRATHI YA KIISLAMU

Kamati ilipitia na kuchambua *Kanuni za Mirathi ya Kiislamu* ambazo zimetungwa chini ya kifungu cha *67(1)* cha *Sheria ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, nambari 2 ya mwaka 2007*. Kifungu hiki kimempa uwezo *Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora* kutunga Kanuni hizi.

Kamati imebaini mambo mbalimbali kama ifuatavyo:

(a) **Yaliyobainika katika Sheria ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, nambari *2* ya mwaka *2007 juu ya Utungaji Kanuni***

Kifungu cha *15* cha Sheria ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, nambari *2* ya mwaka *2007*, kimeipa uwezo Bodi ya Uongozi wa Kamisheni kutunga Kanuni katika Maeneo yafuatayo:

- Kanuni za Utumishi za Kamisheni *{kifungu cha 15 (1)}.*
- Kanuni nyenginezo ambazo ni muhimu kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa majukumu ya Kamisheni *{kifungu cha 15 (2)}.*

Majukumu hayo ya Kamisheni, yameanishwa katika Kifungu cha *4* cha Sheria hiyo ambayo ni:

(i) Kusimamia Mali za Wakfu, Mali za Amana na Mali za Maiti.

(ii) Kuratibu shughuli za Hija zinazohusu Mahujaji kutoka Zanzibar na kuratibu watu binafsi, taasisi au vikundi vinavyotoa huduma za kusafirisha mahujaji.

(iii) Kuratibu na kuweka utaratibu wa Kikanuni kuhusu utoaji, ukusanyaji na ugawaji wa Zakka na sadaka ambazo zinazotolewa kwa madhumuni ya kidini.

(iv) Kuratibu sala na Mabaraza ya Idd ya Kitaifa.

(v) Kanuni zinazohusu ada na tozo zinazokusanywa kutokana na huduma mbali mbali zinazotolewa na Kamisheni ambazo amepewa uwezo Mheshimiwa Waziri kuzitunga. *{kifungu cha 67 (2)}.*

Kamati ilitaka kupata ufafanuzi iwapo Kanuni hizo zimeshatungwa ambapo ufafanuzi ulitolewa na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kama ifuatavyo:

Nam.	Kanuni	Utekelezaji
1.	Kanuni za Utumishi za Kamisheni.	Bado hazijatungwa kutokana na matakwa ya Sheria ya Utumishi wa Umma, nambari *2* ya mwaka *2011* kuwa masuala yote ya utumishi wa umma yatakuwa chini ya Sheria hii pamoja na Kanuni zake.
2.	Kusimamia Mali za Wakfu, Mali za Amana na Mali za Maiti.	Kanuni zimeshatungwa na zinatumika.
3.	Kuratibu shughuli za Hija zinazohusu Mahujaji kutoka Zanzibar na kuratibu watu binafsi, taasisi au vikundi vinavyotoa huduma za kusafirisha mahujaji.	Zinatayarishwa.
4.	Kuratibu na kuweka utaratibu wa Kikanuni kuhusu utoaji, ukusanyaji na ugawaji wa Zakka na Sadaka ambazo zinazotolewa kwa madhumuni ya kidini.	Rasimu ya kwanza ya Kanuni imeshakamilika.
5.	Kuratibu sala na Mabaraza ya Iddi ya Kitaifa	Kanuni zake hazijatungwa kutokana na kwamba Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Mufti Zanzibar, nambari *9* ya mwaka *2001* inafanyiwa marekebisho ambapo jambo hili linatarajiwa

		kujumuishwa katika Sheria hiyo.
6.	Kanuni zinazohusu ada na tozo zinazokusanywa kutokana na huduma mbali mbali zinazotolewa na Kamisheni.	Zimeshatungwa na tayari zinatumika.

(b) **Mapungufu yaliyobainika na Kamati katika Kanuni za Mirathi ya Kiislamu, *2016***

Kamati, ilibaini mambo yafuatayo kwenye Kanuni za Mirathi ya Kiislamu za mwaka *2016*:

Nam.	**Mapungufu**	**Maelezo ya Ufafanuzi**	**Kanuni Inayohusika**
1.	Mgongano wa Kanuni na Sheria nyengine.	Kwenye kifungu kinachohusu adhabu za makosa ambazo hazikutajwa katika Sheria Mama, imebainikia kifungu hicho kinagongana na kifungu cha 42 (e) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria Namba 7 ya mwaka 1984 ambacho kimeweka muongozo kuwa adhabu ya namna hiyo isizidi faini ya Shilingi elfu saba au kifungo kisichozidi miaka miwili, au vyote viwili faini kama hiyo na kifungo kama hicho.	Kanuni ya *15.*
2.	Kukosekana kwa tafsiri ya baaadhi ya maneno.	Baadhi ya maneno yametumika kinyume na yalivyowekwa katika kifungu cha 2 cha Kanuni, mfano neno **"Watoto wadogo"** halijatafsiriwa wakati kwenye tafsiri kuna neno **"Mtoto"** limepewa tafsiri.	Kanuni ya *12 (2).*
3.	Makosa ya Kiuandishi na kiuchapaji.	Vifungu kadhaa vimebainika kuwa na makosa ya kiuandishi, kiuchapaji, sarufi na upangaji wa vifungu ambao unaweza kuleta mkanganyiko wa maana (ambiguity).	Kanuni ya *3, 7 (1), 8(5), 9(3), 10 (4), 11 (1), 12(2), 15* (d).

Nam.	Mapungufu	Maelezo ya Ufafanuzi	Kanuni Inayohusika
4.	Lugha ngumu isiyo rafiki au yenye utata.	Vipo vifungu havifahamiki makusudio yake kwa msomaji wa kawaida hivyo vinaweza visifahamike makusudio yake.	Kanuni ya *8 (3), 10 (4) na 12 (2).*
5.	Makosa yanayohusu Jaduweli zilizowekwa katika kanuni.	Jaduweli kumi na mbili zimeambatanishwa na kanuni hizi kamati na imebainikuwa: *(a)* Rejea (references) za Jaduweli katika vifungu vya kanuni hazikufanyika sawasawa. *(b)* Mapungufu katika uwekaji na mpangilio wa maneno, maelezo, nambari na kolamu. *(c)* Kuna mchanganyiko wa lugha ya Kiswahili na Kingereza ambapo baadhi ya Jaduweli zimewekwa kwa lugha kingereza nyengine kwa Kiswahili. Aidha zipo Jaduweli zimewekwa kwa lugha ya Kiswahili lakini ndani zimechanganywa na maneno ya Kingereza bila maneno hayo kutafsiriwa. Vile vile yapo maneno yamechanganywa lugha zote mbili mfano**"kesi namba"**. *(d)* Yamewekwa maneno ambayo hayamo kwenye tafsiri, mfano neno **"Mrathi"** wakati kwenye tafsri limetafsiriwa neno **"Mrithiwa"** na **"Afisa Urithi".**	Kanuni ya *8 (5)* na Jaduweli ya *1* mpaka Jaduweli ya *12*.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAPENDEKEZO NA MAONI YA KAMATI

Baada ya maelezo hayo kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo inatoa mapendekezo na maoni yafuatayo:-

3.1 KUIJENGEA UWEZO KAMATI

a. Kamati ipatiwe mafunzo zaidi ya kujengewa uwezo kwa kufanya ziara katika Bunge la Jamhuri ya Muungano na kukutana na Kamati ya Sheria ndogo ya Bunge; pamoja na Ofisi ya Baraza la Wawakilishi kumleta Mkufunzi kutoka Bungeni, bado Wajumbe pamoja na Sekretarieti wanahitaji zaidi kupata fursa ya kubadilishana mawazo na uzoefu kuhusu uendeshaji wa Kamati ya Bunge ya Kanuni na Sheria Ndogo.
b. Kamati ipewe uzito wa aina yake kama zilivyo Kamati nyengine, isichukuliwe kuwa ni Kamati ndogo isiyo na kazi nyingi.
c. Kamati kupewa mafunzo zaidi yanayohusu mambo mbali mbali ya Kanuni na Sheria ndogo ndogo ili kuimarisha zaidi uwezo wa wajumbe waweze kumudu vyema shughuli zao za Kamati.

3.2 UTUNGAJI WA KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO KWA WIZARA NA TAASISI ZAKE

Kamati inapendekeza yafuatayo:-

a. Ofisi ya Baraza la Wawakilishi itoe taarifa na tamko rasmi kwa Wizara/Taasisi za Serikali pamoja na Kamati za Kisekta za Baraza juu ya kuanza rasmi kwa shughuli za Kamati na kuanza kufuata taratibu za utungaji wa Kanuni.
b. Kamati inazishauri Kamati za kisekta wakati zinapofuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara zao, kuhakikisha kwamba wanatambua Sheria zinazosimamiwa na Wizara na kuhakikisha Kanuni za Sheria hizo zinatungwa kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha.
c. Wizara na Taasisi zinazokasimiwa mamlaka na Baraza la Wawakilishi zihakikishe zinatunga Kanuni kwa muda muafaka mara tu baada ya kutungwa kwa sheria zinazowahusu.
d. Kanuni na Sheria ndogo zinazotungwa na Wizara au Taasisi zinazohusika zihakikishe kuwa zinazingatia hatua muhimu za utungaji na kufuata misingi ya Katiba na haki za binaadamu wakati wa uandishi. Aidha, pia Kanuni ziendane na masharti ya Sheria mama na sheria nyengine za nchi ili kuepusha migongano isiyo ya lazima.

e. Wizara na Taasisi ziwajengee uwezo Wanasheria wake katika taaluma ya utayarishaji na utungaji wa Kanuni na Sheria ndogo ndogo kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali au kwengineko na pia kuwashirikisha kikamilifu katika kazi za kutengeneza kanuni katiak Taasisi zao.
f. Wizara/Taasisi zitunge Kanuni na Sheria ndogo ndogo kwa kutumia lugha fasaha, nyepesi na rafiki itakayowezesha walengwa kuifahamu kwa urahisi.
g. Sheria ya Tafsiri ya Sheria, nambari 7 ya mwaka 1984 inahitaji kufanyiwa mapitio ili kuangalia mapungufu yaliyomo na hatua za kuifanyia marekebisho ziweze kuchukuliwa.

3.3 UFANISI KATIKA UTENDAJI KAZI WA KAMATI

Kamati katika eneo hili inapendekeza yafuatayo:-

a. Kanuni ya *33(4) ya Kanuni za Kudumu za Baraza*, inaonekana wazi kwamba ni kikwazo katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwani imeweka muda maalumu na mfupi kwa Kamati kuweza kupitia Sheria ndogo/Kanuni zitakazoletwa Barazani. Hivyo, Kamati inapendekeza Baraza lihakikishe kuwa kanuni hiyo inafanyiwa marekebisho kwa haraka. Katika muda ambao kanuni hii haijarekebishwa, Kamati italazimika kuwekewa utaratibu maalumu; kwani itapaswa kuzifanyia kazi Kanuni zitakazofikishwa Barazani mara moja ili kukidhi masharti ya kanuni hiyo. Kwa utaratibu huo tu ndio Kamati itaweza kuzipitia, kuzichambua na kutoa mapendekezo Barazani ndani ya muda wa miezi *mitatu* iliyowekwa chini ya kanuni ya *33(4)*.
b. Utaratibu wa Kamati uwe tofauti na mzunguko wa kawaida wa Kamati nyengine za Kisekta ili kuepusha mgongano wa Wajumbe wa Kamati, ni vyema shughuli za Kamati hii zikatangulia kuanza ili kuendana na muda wa Kikanuni.
c. Ikiwezekana Kanuni ya Baraza itowe uwezo kwa Kamati iwe na uwezo wa kupitia na kuzichambua hata Kanuni na Sheria ndogo ndogo zilizotungwa miaka ya nyuma (Kama ilivyo katika Mabunge mengine) hususan zile Kanuni zinazoleta kero au kulalamikiwa na wananchi.
d. Sekretarieti ya Kamati Kamati ni vyema iangaliwe zaidi kimaslahi kwa zile kazi za maandalizi ya awali za Kamati huwa zinahitaji muda wa ziada nje ya muda wa kawaida wa Kamati.

   Kwa kuwa:

- Sekretarieti katika utekelezaji wa kazi zake ili ziwe na ufanisi itapaswa kuzipitia na kufanya uchambuzi wa awali wa Kanuni au Sheria.
- Sekretarieti itapaswa kuandaa Jaduweli kuhusu matokeo ya uchambuzi wao wa Kanuni/Sheria Ndogo kabla ya kukutana na Wajumbe wa Kamati.

Pamoja na mapendekezo hayo Kamati ilishauriwa kuzipitia na kuzichambua Kanuni mara tu baada ya kutungwa kama ilivyo kwa utaratibu wa kutunga Sheria ili kupunguza uwezekano wa kubatilisha Kanuni baadaye.

4. HITIMISHO

Kazi za Kamati hii zimejumuisha Wajumbe kutoka Kamati nyengine za Kisekta za Baraza la Wawakilishi, ambao wanalazimika kujigawa katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati hii. Kazi kubwa imefanywa na wajumbe hawa hadi ripoti hii ya awali inachapishwa.

Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo majukumu yake yanategemea uwepo wa Kanuni muda wote, hivyo wakati ripoti hii inamaliza kutayarishwa, Kamati ilikuwa inaendelea na hatua za kupitia na kuchambua Kanuni za Makampuni za mwaka 2017 hivyo taarifa kuhusu uchambuzi wa Kanuni hizo itawasilishwa katika vikao vinavyofuata.

Kamati inatoa shukurani zake za dhati Spika wa Baraza la Wawakilishi kwa kuwezesha kuipatia fursa ya kutekeleza majukumu yake katika kipindi hiki kifupi.

Kamati pia inatoa shukurani zake za dhati kwa viongozi na watendaji wote wa Taaisi zifuatazo:-

a. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mkuu wa Serikali;
b. Tume ya Kurekebisha Sheria;
c. Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar;
d. Taasisi zisizo za Kiserikali;
e. Baraza la Manispaa Mjini;
f. Baraza la Manispaa Magharibi A;
g. Baraza la Manispaa Magharibi B;
h. Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ;
i. Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Pia Shukurani za pekee ziende kwa Wajumbe wote wa kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya uchambuzi wa Kanuni zilizowasilishwa na hatimaye kukamilisha kazi (ripoti) hii. Aidha kwa dhati kabisa Kamati inawashukuru watumishi wa Baraza la Wawakilishi chini ya Uongozi wa Katibu wa Baraza kwa mashirikiano wanayoipatia Kamati katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, shukrani kwa Makatibu Kamati wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo kwa kazi kubwa ya kuratibu shughuli za Kamati na matayarisho ya ripoti hii mpaka kukamilika kwake.